Australian Government

Department of Home Affairs

# Privacy notice

## Notisi ya faragha

Form
1442i SWA
SWAHILI

Department of Home Affairs (Idara ya Mambo ya Ndani) (Idara) ni pamoja na Jeshi la Mpakani wa Australia. *Privacy Act 1988* (Privacy Act) *(Sheria ya Faragha 1988)* inahitaji Idara kujumlisha mtu binafsi kuhusu mambo fulani inapokusanya taarifa binafsi kuhusu yeye. Fomu hii ni taarifa kwako kuhusu mambo hayo.

## Taarifa binafsi ni nini?

Sheria ya Faragha inaeleza kwamba taarifa binafsi ni taarifa au maoni kuhusu mtu binafsi ambaye anaweza kutambuliwa ya kutosha.

Idara pia inakusanya taarifa binafsi fulani yenye siri, inayoelezwa chini ya Sheria ya Faragha na ni pamoja na taarifa kuhusu asili ya mbari au kabila ya mtu binafsi, ujinsia au matendo ya kipenzi, kumbukumbu za jinai, taarifa ya afya na ya biometric, ujumbe wa mashirika ya ueledi au biashara, imani au uhusiano wa dini, imani ya falsafa, na ujumbe wa mashirika ya siasa.

Vipengele vikuu vya sheria vinavyosimamiwa na Idara ni *Migration Act 1958* (the Migration Act) *(Sheria ya Uhamiaji Australia 1958* (Sheria ya Uhamiaji)), *Customs Act 1901* (the Customs Act) *(Sheria ya Forodha 1901* (Sheria ya Forodha)), *Immigration (Guardianship of Children) Act 1946* (the IGOC Act) (*Sheria ya Uhamiaji (Ulezi wa Watoto) 1946* (Sheria ya IGOC)), *Excise Act 1901* (the Excise Act) (*Sheria ya Ushuru 1901* (Sheria ya Ushuru)), *Australian Border Force Act 2015* (the Border Force Act) *(Sheria ya Jeshi la Mpakani la Australia 2015* (Sheria ya Jeshi la Mpakani)), *Maritime Powers Act 2013* (Maritime Powers Act) *(Sheria ya Mamlaka ya Bahari 2013* (Sheria ya Mamlaka ya Bahari)), na *Australian Citizenship Act 2007* (Citizenship Act) (*Sheria ya Uraia wa Australia 2007* (Sheria ya Uraia)).

### Vitambulisho binafsi

Sheria za Uhamiaji na Uraia ni pamoja na utoaji huduma maalum kuhusu ukusanyaji, utumiaji, na/au ufunuzi wa taarifa zako binafsi, pamoja na taarifa siri kama biometrics (zinazojulikana pia kama 'vitambulisho binafsi').

Sheria hizo zinaeleza vitambulisho binafsi kuwa pamoja na:

- alama za vidole au za mikono
- picha ya uso na mabega
- kumbukumbu ya sauti au video (kwa malengo ya Sheria ya Uhamiaji tu pamoja na mambo kadhaa ya kipekee)
- upimiaji wa urefu na uzito
- skani ya mboni
- sahihi ya mtu, au
- utambulisho wowote wengine unaoagizwa katika kanuni.

Taarifa ya biometric (vitambulisho binafsi) inaweza kukusanywa na/au kuthibitishwa kwa watu binafsi:

- kwenye viwanja vya ndege wakati wa kusafiri
- kwa waombaji wa viza nchini (pamoja na mwombaji wa viza ya ulinzi)
- ambao sio raia katika jumuiya ya Australia
- ambao wamo kizuizini
- ambao ni waombaji wa uraia wa Australia.

## Nini Idara inachofanya na habari za mawasiliano yetu

Dhamira ya Idara ni kulinda mpaka wa Australia na kusimamia mzunguko wa watu na bidhaa nchini kwa kuchangia na kuhakikisha:

- siku za baadaye za Australia kwa kupitia uhamiaji unaosimamiwa
- kulinda wakimbizi na kuchangia kwa sera ya huruma kimataifa
- usalama wa Australia kupitia usimamiaji wa mpaka na huduma za wasafiri
- ukusanyaji wa ushuru wa mpaka na takwimu wa biashara
- kurahisisha biashara halii
- faida za usalama wa bahari na wa kichumi wa Australia
- kutekeleza sheria za uhamiaji za Australia na ukamilifu katika kufanya uamuzi
- kusimamia sheria za uraia za Australia.

Habari nzima zote zinaweza kupatikana kwa tovuti ya Idara kwa **www.homeaffairs.gov.au**

Kama ukiamini kwamba tumekusanya au kutumia taarifa zako vibaya, waweza kufanya yafuatayo:

- jaza fomu ya kutoa maoni mtandaoni kwenye **www.homeaffairs.gov.au/feedback**
- andika kwa:
  The Manager
  Global Feedback Unit
  GPO Box 241
  Melbourne VIC 3001
  Australia

## Idara itakusanya taarifa binafsi kutoka nani

Kwa ujumla, Idara (au watoaji wake wa huduma wa mkataba) itakusanya taarifa zako binafsi moja kwa moja kutoka kwako, mshiriki mwingine unaoipa mamlaka kutenda kwa niaba yako au mfumo mwenye mamlaka unaotambulishwa chini ya Sheria ya Uhamiaji. Mifumo yenye mamlaka ni pamoja na SmartGate na mifumo mingine ya otomatik ya kuangalia uvukaji mpaka. Tunaweza pia kukusanya taarifa zako kutoka kwa upande wa tatu ambao inawezekana kuwa ni pamoja na mashirika mengine ya Serikali ya Australia, mashirika ya kutekeleza sheria, serikali za nje, wafadhili, madaktari, mashirika ambao umeteua, watoaji wa elimu, waajiri na wanajamii wanaowasiliana na Idara na habari (km. 'simu ya kumshtaki mwingine').

### Mashirika au kontrakta wanaotoa huduma za uhamiaji

Taarifa binafsi kadhaa zinakusanywa na kutumiwa kwa niaba yetu na mashirika mengine ya serikali yanayoruhusiwa kufanya baadhi ya kazi ya Idara.

Taarifa binafsi pia zinakusanywa na kutumiwa kwa niaba yetu na makandarasi. Mifano ni pamoja na kushughulika abiria wa juu na mashirika ya safari za ndege zote safari za kutoka na kuingia, mifumo ya kompyuta, maswali/mahoji ya utafiti, huduma za msaada kwa watu wanaokuwepo uziuzi wa uhamiaji na huduma za uganga.

Idara inahitajika kwamba makandarasi yake pia wanatii Sheria ya Faragha, bila kujali wapo nchini Australia au wapo n'gambo.

© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2020

## Ukusanyaji wa taarifa zako binafsi ambazo unahitaji au kuruhusu na sheria

Sheria ya Uhamiaji, Sheria ya IGOC, Sheria ya Forodha, Sheria ya Ushuru, Sheria ya Mamlaka ya Bahari, Sheria ya Uraia na Sheria ya Faragha zinaruhusu, na katika hali kadhaa yanahitaji, Idara kukusanya taarifa binafsi fulani ili kusimamia sheria hizo.

### Sheria ya Uhamiaji

Kuhusu maombi ya viza, Idara:

- inaruhusu kukusanya taarifa zozote zinazofaa kwa ombi (angalia kifungu 56 cha Sheria ya Uhamiaji), na
- inaweza kukulazimisha kutoa utambulisho binafsi (angalia vifungu namba 40 na 46 vya Sheria ya Uhamiaji).

Waombaji wa viza, na baadhi ya wamiliki wa viza, lazima waijulishe Idara badiliko katika hali au taarifa zisizo sahihi zilizotolewa kwenye fomu ya ombi (vifungu namba 104 na 105 vya Sheria ya Uhamiaji).

Idara inaweza kukuhitaji kutoa kitambulisho binafsi kimoja au zaidi kwa malengo ya Sheria ya Uhamiaji na Kanuni za Uhamiaji 1994.

Wakati unapotoka Australia, Idara inaweza kukuhitaji kutoa vitambulisho binafsi fulani (angalia kifungu namba 257A cha Sheria ya Uhamiaji).

Kutambua watu wasio raia wasio halali, Idara inaweza kuhitaji:

- ushahidi wa utambulisho na hali ya viza, pamoja na utambulisho binafsi (angalia kifungu namba 188 cha Sheria ya Uhamiaji)
- mtu kutoa hati au maelezo kuhusu nafsi au mahali pa mtu mtuhumiwa kuwa sio raia na sio halali (angalia kifungu 18 cha Sheria ya Uhamiaji).

Mtu ambaye yumo kizuizini cha uhamiaji atoe vitambulisho binafsi (angalia vifungu namba 258 na 261AA(1) ya Sheria ya Uhamiaji na kanuni 3.30 ya Kanuni ya Uhamiaji).

Katika mazingira ya wafadhili wa biashara, Idara na Fair Work Ombudsman (FWO) (Mchunguzi Mkuu wa Kazi Sawa (FWO)) inaweza kukusanya taarifa binafsi kufuatilia na mamlaka ya uchunguzi ya Kipengele kidogo F cha Kipengele cha 3A ya Sehemu 2 ya Sheria ya Uhamiaji.

Kwa kusudi ya mamlaka ya uchunguzi katika kifungu 252 ya Sheria ya Uhamiaji, afisa aliye na mamlaka anaweza kuhifadhi hati au kitu kingine kinachopatikana na mtu au katika mali chini ya utawala ya mtu, kwa mfano, kinachoweza kuwa ushahidi kufuta viza ya mtu.

Afisa anaruhusiwa kushika hati ya uwongo ambayo aliipoteza (soma kifungu cha 487ZJ, na Kipengele cha 1 cha Sehemu 9 ya Sheria ya Uhamiaji pamoja na jinsi ya kushughulikia hati).

### Sheria ya Uraia

Idara inaweza kukusanya taarifa binafsi mbalimbali kuridhishwa kwamba mtu binafsi anatimiza masharti ya uraia.

Tuna mamlaka kuomba utambulisho binafsi kulingana na maombi ya uraia, na ombi haliwezi kukubaliwa kama mwamuzi hairidhishwa utambulisho wako (angalia Kipengele namba 5 cha Sehemu 2 na sehemu za 17(3), 19D(4), 24(3), na 30(3) ya Sheria ya Uraia).

Mwakilishi anaruhusiwa kushika hati ya uwongo ambayo aliipotezawa (soma kifungu 45B, na Kipengele cha 1 kati Sehemu 3 ya Sheria ya Uraia pamoja na jinsi ya kushughulikia hati).

### Sheria ya IGOC

Chini ya *Immigration (Guardianship of Children) Act 1946* (the IGOC Act) (*Sheria ya Uhamiaji (Ulezi wa Watoto) 1946* (Sheria ya IGOC)) na kanuni zake, Waziri wa Uhamiaji ni mlezi wa watoto fulani wasio raia na wanaowasili nchini Australia pasipokuwa na mzazi au mlezi mwenye umri wa miaka 21 au zaidi (inayojulikana kama watoto wa IGOC chini ya umri wa miaka 18).

Kusaidia kutekeleza majukumu wa kimalezi, sheria ya IGOC inamruhusu Waziri kuwakabidhi mamlaka na shughuli zake za kimalezi kuteuwa afisa wa serikali ya Jumuiya ya Madola au jimbo au wilaya (hujulikana kama 'walezi wawakilishi'). Watu au mashirika yenye utayari na yanayofaa wanaweza pia kuteuliwa kuwa 'watunzaji' wa watoto wa IGOC. Kwa maneno ya jumla, mtunzaji ana haki na jukumu kufanya maamuzi kuhusu malezi na maamuzi ya kila siku ya mtoto ambaye yuko kwenye uangalizi wake.

Kuhakikisha malezi na ustawi ya kila siku kwa watoto chini ya Sheria ya IGOC, Idara inakusanya taarifa binafsi kuhusu watoto wa IGOC na watunzaji wao. Kuhakikisha mahitaji ya utunzaji na ustawi wa kila siku wa watoto wa IGOC yanaridhisha, inapohitajika na kufuata Sheria ya Faragha, Idara inaweza kufichua taarifa binafsi kwa, na kukusanya taarifa kutoka:

- mamlaka ya jimbo/ wilaya, pamoja na mashirika ya ustawi wa watoto
- walezi wakilishi
- watunzaji
- wazazi, watunzaji na/au wanafamilia, na/au
- mashirika mengine ya Serikali ya Australia.

### Sheria ya Forodha na Sheria ya Ushuru

Idara inaruhusiwa kukusanya anuwai ya taarifa binafsi na za kibiashara katika usimamiaji wa Sheria za Forodha na za Ushuru na sheria nyingine zinazohusika za Australia (pamoja na Sheria ya Uhamiaji na sheria za ushuru). Hasa, Idara inakusanya taarifa hiyo katika kulinda mipaka ya Australia na kuhakikisha ukusanyaji wa mapato ya mipaka.

Wakati mwingine, fomu zetu zinazokusanya taarifa binafsi kutoka kwako kuhusu mambo yanayotokana na Sheria za Forodha na Ushuru na sheria za ushuru zinaweza pia kuonyesha notisi ya ukusanyaji ya pekee. Fomu pia zitakupatia na taarifa maalum kuhusu ukusanyaji, utumiaji, na ufunuzi wa taarifa binafsi inayokusanyika katika maandishi hayo, na zisomewa pamoja na notisi hii ya faragha.

Kwa mfano, chini ya vifungu vya 64ACA na 64ACB wa Sheria ya Forodha, Idara inahitajika kukusanya taarifa binafsi fulani kuhusu abiria na wafanyakazi wa meli na ndege ambao wanawasili nchini Australia, kwa malengo ya kusimamia Sheria ya Forodha, Sheria ya Uhamiaji na sheria zingine.

### Sheria ya Mamlaka ya Bahari

Idara inaruhusiwa kukusanya taarifa binafsi katika kutumia mamlaka ya bahari na mashirika ya kutekeleza sheria baharini. Mamlaka hizo zinasaidia kutekeleza sheria za Australia zinazohusu bahari, pamoja na kuhusika na uvuvi haramu wa kigeni, forodha, mapambano dhidi ugaidi baharini, uhamiaji, karantini na usafirishaji wa dawa za kulevya, na pia makubaliano na mipango ya kimataifa baharini.

### Sheria ya Faragha

Sheria ya Faragha inaruhusu ukusanyaji wa:

- taarifa za siri zinaporuhusiwa chini ya sheria, au kwa kazi inayohusu kutekeleza sheria, au kwa idhini yako
- taarifa binafsi nyingine inapokuwa lazima kwa, au kuhusiana moja kwa moja, kazi au shughuli moja au zaidi ya Idara.

### Sheria ambazo zinazingatia Idara kuwa shirika la kutekeleza sheria

Idara ni shirika la kutekeleza sheria kwa malengo fulani chini ya Sheria zifuatazo: the *Crimes Act 1914,* the *Criminal Code Act 1995,* the *Australian Nuclear Science and Technology Organisation Act 1987* (the ANSTO Act) and the *Independent National Security Legislation Monitor Act 2010* (*Sheria ya Makosa ya Jinai 1914, Sheria ya Kanuni ya Adhabu ya Jinai 1995, Sheria ya Shirika ya Sayansi ya Nyuklia na Teknolojia 1987* (Sheria ya ANSTO) na *Sheria ya Kuangalia kwa Uhuru Sheria ya Usalama wa Taifa 2010*)), na inaweza kukusanya taarifa binafsi ili kufanya kazi na shughuli zake chini ya Sheria hizo.


© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2020

## Kusudi tunakokusanya taarifa zako binafsi

Kusudi letu kuu kukusanya taarifa binafsi ni kufanya kazi au shughuli za Idara zinazohusu mienendo yako ya njia ya uhamiaji na/au uraia, pamoja na harakati za bidhaa katika mpaka. Tunasimamia shughuli zifuatazo:

- viza na uhamiaji
- forodha na ushuru, pamoja na usimamizi wa sheria zingine fulani za Australia pamoja na za ushuru, afya, karantini, uchumi, jinai, mali ya kiakili na sheria za ulinzi wa jumuiya
- usaidizi wa wakimbizi na huruma
- utawala wa mipaka
- kufuatana na viza na utatuzi wa hali ya uhamiaji
- uzuizi wa uhamiaji, kuondoa au kuhamia kwa Kituo cha Utengenezaji wa Mkoa (ikiwa ni pamoja na watoa huduma na mamlaka ya nje kwa msaada wa usindikaji wa shughuli za eneo lililo mbali ya pwani, kama vile utekelezaji wa sheria, utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na makazi)
- uraia.

Taarifa unazotoa katika ombi la viza, ufadhili, biashara, bidhaa ziingiazo ndani na bidhaa toka ndani kwenda nje, karantini, au uraia zitatumika kwa kusudi hilo maalumu.

Chini ya Sheria ya Faragha, taarifa inaweza kutumika kwa kusudi la pili. Kwa jumla, hii inatokea unapotazamia ya kiasi kwa Idara kutumia au kufichua taarifa zako binafsi na kusudi kwa pili ni chochote kuhusu moja kwa moja kwa kusudi kuu (kwa taarifa siri) au kuhusu kusudi kuu (kwa taarifa binafsi nyingine). Kwa mfano, taarifa unazotoa katika ombi la viza zinaweza kutumiwa kuhusu maombi yako ya fuatia (pamoja na chini ya *Freedom of Information Act 1982 (Sheria ya Uhuru wa Taarifa 1982)* na Sheria ya Faragha). Zaidi, tunaweza kutumia habari za mawasiliano ya elektroniki ulizotolewa kuwasiliana nawe kuhusu maswala ya uhamiaji.

## Matokeo kama taarifa zako binafsi hazikusanywi na Idara

Kama taarifa zako binafsi hazikusanywi, Idara inaweza kushindwa kushughulika ombi lako la viza au uraia au (kama ikifaa) kushindwa kutoa hudumu za msaada wa biashara, bidhaa ziingiazo ndani, bidhaa kwenda nje, na karantini kwa ajiri yako.

Kushindwa kukusanya taarifa zako kunaweza kuzuia uwezo wa Idara kutimiza wajibu wake kisheria (hasa kuhusu utii), majukumu yake ya jibu ya huduma, au ahadi ya mataifa ya Australia.

## Ufunuzi wa kawaida wa taarifa zako binafsi kwa upande wa tatu

### Ufunuzi kwa wakala walioteuliwa

Kama umeteuliwa mtu, kama mwanafamilia, wakala wa uhamiaji, wakala wa usafiri wa ndege, wakala wa forodha, Mchunguzi Maalum, Mbunge, au mwanasheria kuwa mwakili wako, taarifa zako binafsi zinaweza kufichuliwa kwa upande wa tatu wale endapo umeomba kwamba tusifanye hivyo.

Taarifa zako binafsi zinaweza kufichuliwa kwa mtu unayefadhili au mfadhili wako.

### Ufunuzi wa kawaida kwa Mashirika mengine ya Serikali

Idara, katika hali fulani, inaruhusiwa chini ya Sheria ya Jeshi la Mpakani au utungaji sheria nyingine kufichua taarifa binafsi kwa mashirika mengine ya serikali, kwa mfano kwa malengo ya kuendesha kazi na shughuli zake, au kuwezesha au kusaidia shirika lingine kufanya kazi zake. Mifano ni pamoja na ufunuzi kuhakikisha utambulisho wako, kuhakikisha ukweli wa hati ulizotoa, kulinganisha ufanano wa data, au kusimiamia majukumu ya utii.

Mashirika ya serikali ambayo tunabadilishana taarifa ni pamoja na, lakini bila kikomo kwa:

- Idara ya Huduma ya Binadamu (DHS), kuendesha *Social Security Act 1991 (Sheria ya Usalama ya Jamii 1991),* the *Child Support (Assessment) Act 1989 (Sheria ya Msaada kwa Watoto (Kadirio) 1989)* na *Child Support (Registration and Collection) Act 1988 (Sheria ya Usaidizi wa Watoto (Kuandikisha na Kukusanya) 1988)*
- Idara ya Huduma ya Jamii
- Idara ya Kilimo, kuendesha mfumo ya biosecurity ya Australia na uendeshaji wa *Quarantine Act 1908 (Sheria ya Karantini 1908), Export Control Act 1982 (Sheria ya Kudhibiti Bidhaa kwenda nje 1982)* na *Imported Food Control Act 1992 (Sheria ya Kudhibiti Chakula Kiingizwacho 1992)*
- Usimamizi wa Bidhaa za Kimatibabu
- Idara ya Tasnia, Uvumbuzi na Sayansi
- Australian Sports Anti-Doping Authority (Mamlaka Michezo ya Australia ya Kupinga-Dawa za Kulevya kusimamia National Anti-Doping Scheme (Mpango wa Kitaifa wa Kupinga-Dawa ya Kulevya)
- Idara ya Elimu, kuendesha *Education Services for Overseas Students Act 2000 (Sheria ya Huduma za Elimu kwa Wanafunzi wa Ng'ambo 2000)*
- Idara ya Tasnia, Uvumbuzi na Sayansi
- Idara ya Mambo ya Askari Wastaafu, kusimamia *Veterans' Entitlements Act 1986 (Sheria ya Stahiki wa Askari Wastaafu 1986*)
- Ofisi ya Ushuru wa Australia (ATO), kusimamia *Income Tax Assessment Act 1997 (Sheria ya Tathimini ya Ushuru wa Kipato 1997) na sheria nyingine za ushuru*
- Mchunguzi Mkuu wa Usawa katika kazi (FWO), kusimamia *Fair Work Act 2009 (Sheria ya Kazi Sawa 2009)*
- Idara ya Mambo ya Nchi za Nje na Biashara (DFAT), kuendesha *Australian Passport Act 2005 (Sheria ya Pasi ya Australia 2005)* na kupata taarifa ya nchi kwa kushughulikia viza ya ulinzi, na kuhusu pasi yoyote ya nje unayoweza kustahili kumiliki kama raia ya mataifa mawili
- Tume la Kupiga Kura ya Australia, kusimamia *Commonwealth Electoral Act 1918 (Sheria ya Kupiga Kura ya Jumuiya ya Madola 1918)*.

### Mashirika ya Ukaguzi, Ukaguzi wa Mahesabu na Uchunguzi

Kama ukiomba kwa ukaguzi wa ustahili au wa jaji wa uamuzi, Idara itatoa taarifa binafsi za kufaa kwa baraza au makahama inayofanya ukaguzi.

Tunashirikisha taarifa na mashirika ya uchunguzi kama:

- Mchunguzi Maalum wa Jumuiya ya Madola
- Ofisi ya Kamishna wa Taarifa ya Australia
- Ukaguzi wa Mahesabu wa Australia ya Kitaifa
- Tume ya Haki za Binadamu ya Australia
- Mchunguzi Maalum wa Kazi Sawa.

### Dharura na kutekeleza sheria

Taarifa binafsi zinaweza kutolewa kwa mashirika ya kutekeleza sheria au huduma za dharura katika wakati wa dharura, majeraha makali au kifo.

Idara pia inafichua taarifa kwa mashirika ya kutekeleza sheria ya Australia (Jumuiya ya Madola, jimbo na wilaya) na nchi za nje inapohitajika kwa kutekeleza sheria ya jinai, pamoja na kuzuia, kugundua, kuchunguza na kushtaki au adhabu ya kosala jinai.

### Miradi ya msaada

Taarifa inayokusanywa katika kushughulika viza inaweza kufichuliwa kwenye:

- Idara ya Huduma ya Jamii kutoa usaidizi ya makazi
- Idara ya Tasnia, Uvumbuzi na Sayansi kusaidia na kufuatia mafunzo ya lugha ya Kiingereza..

### Ufunuzi kwa mamlaka ya leseni

Kama ukiomba leseni nchini Australia, Idara inaweza kufichua taarifa kuhusu hali yako ya uhamiaji na ustahili wa kufanya kazi kwa mamlaka husika, na katika visa kadhaa kama umepewa uraia wa Australia. Taarifa hizi zitatumika kutathmini kama unafaa kumiliki leseni. Pia kuna ufunuzi maalum unaoweza kufichua kama ukiomba leseni maalum chini ya Sheria ya Forodha.

### Ufunuzi wenye ruhusu wa taarifa binafsi

'Utambulisho binafsi' unajieleza Ukurasa wa 1.

Idara ina mamlaka chini ya Sehemu 4A ya Sheria ya Uhamiaji na s43 ya Sheria ya Uraia kufichua vitambulisho binafsi katika hali mbalimbali. Mifano ni pamoja na:

- kuhakikisha hali ya uraia na viza
- kutekeleza sheria ya jinai
- kubadilishana taarifa inayotambulisha mtu chini ya mpangalio na shirika la Serikali ya Australia
- kupatikana taarifa zinazofaa kwa mahakama, baraza, au shirika la uchunguzi
- inapohitajika na sheria ya Australia.

Idara pia ina mamlaka chini ya Sheria ya Uraia kufichua vitambulisho binafsi kwa makusudi ya sheria ya uraia au uhamiaji.

Sehemu 4A ya Sheria ya Uhamiaji pia inaruhusu Idara kufichua taarifa binafsi (pamoja na vitambulisho binafsi) katika hali ifuatayo:

- kulinganisha data ili:
  - kutambua, au kuhakikisha utambulisho wa mtu
  - kusaidia maendeleleo ya watu ambao wanaingia au kuondoka nchini Australia
  - kutambua watu wasio raia ambao wana historia ya jinai, au shaka kuhusu tabia au ya usalama wa kitaifa
  - kupinga udanganyifu wa hati na wa utambulisho katika mambo ya uhamiaji
  - kusaidia kushughulika viza vya ulinzi
- kutambua au kutambua mahali pa mtu (angalia pia vifungu 33FA na 33FC vya Sheria ya Uhamiaji)
- kwa mashirika ya uchunguzi yaliyoagizwa kama Ofisi ya Ukaguzi wa Mahesabu ya Australia ya Kitaifa na Tume ya Hakiza Binadamu ya Australia
- kufanya mipango na serikali za nje ili kuondoa mtu kutoka Australia au kwa kusudi kwa kurejesha mtu kuja na kutoka Australia kurudi nchi aliyefanya makosa
- kupatikana taarifa kwa serikali zilizotajwa za nje, mashirika ya kutekeleza sheria au kutawala mipaka ya serikali za nje, au mashirika yaliyotajwa ya kimataifa kwa makusudi ya kusimiamia maswala ya uhamiaji (angalia kifungu 5A(3) cha Sheria ya Uhamiaji)
- kupata na kutoa msaada katika mambo ya mataifa ya jinai.

Kwa maelezo zaidi kuhusu vitambulisho binafsi angalia fomu 1243i.

Kuhusiana na viza ya kufanya kazi, Idara inaruhusu pia kufichua taarifa binafsi fulani kuhusu wafadhili au wamiliki wa viza kwa akilinganishwa na mmiliki wa viza au mfadhili (angalia kifungu 140ZH cha Sheria ya Uhamiaji na kanuni 2.103, 2.104 na 2.105).

Idara inaruhusiwa pia kufichua kwa kiasi kidogo sana taarifa binafsi inayokuwa taarifa ya Uhamiaji na Ulinzi wa Mipaka (soma sehemu 4(1) ya Sheria ya Jeshi la Mpakani) katika hali limited inayoelezwa katika Sehemu 6 ya Sheria ya Jeshi la Mpakani. Katika hali fulani, Sheria ya Jeshi la Mpakani inaruhusu ufunuzi kwa washiriki wafuatao:

- mashirika au mamlaka ya Jumuiya ya Madola, jimbo na wilaya
- Polisi ya Shirikisho la Australia (AFP) au jeshi la polisi au huduma ya jimbo au wilaya
- afisa mchunguzi wa vifo
- wamiliki wa ofisi wa sheria za Bunge wa Jumuiya ya Madola, jimbo au wilaya (km. Mchunguzi Mkuu)
- mamlaka au watu wanaoelezwa na Sharti ya Jeshi la Mpakani la Australia (Secrecy and Disclosure) (Siri na Ufunuzi) 2015, kama Shirika ya Msalaba Mwekundu la Australia
- nchi ya nje au shirika la umma la kimataifa.

Hata hivyo, kwa kuongezea na masharti mengine maalum yamo Sehemu 6 ya Sheria ya Jeshi la Mpakani, ufunuzi wa taarifa binafsi chini ya Sheria ya Jeshi ya Mipaka inaruhusiwa tu kwa mojawapo ya mamlaka yaliyotajwa hapo juu kwa 'lengo au malengo yenye ruhusu' kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Jeshi la Mipakani. Kwa mfano taarifa zinaweza kutolewa kwa malengo yafuatayo:

- kusimamia au kutekeleza sheria ya makosa ya jinai au sheria inayohusu biashara
- kusaidia upelelezi, uchunguzi au baraza la utafiti wa sababu ya kifo
- kulinda afya ya umma, au maisha au usalama wa mtu mmoja au watu
- kukusanya au kuhakiki takwimu kwa mujibu wa *Census and Statistics Act 1905 (Sheria ya Census na Takwimu 1905)* au *Australian Bureau of Statistics Act 1975 (Sheria ya Mamlaka ya Takwimu ya Australia 1975)*
- kulinda mapato ya serikali
- kumtambua mtu au kuhakiki uraia wake au viza yake.
- utoaji wa huduma kwa watu wasio raia wa Australia
- usimamizi wa Mpango wa Kitaifa wa Kupambana na Dawa za Kulevya
- lengo linalohusiana na uhamiaji, karantini au udhibiti wa mpaka kati ya Australia na nchi ya nje
- mambo yote yanasimamiwa na sheria ikiwa ni pamoja na Customs Act, Migration Act, Maritime Powers Act, Citizenship Act, IGOC Act, (Sheria ya Forodha, Sheria ya Uhamiaji, Sheria ya Mamlaka ya Bahari, Sheria ya Uraia, Sheria ya IGOC, nk)
- lengo linalohusu ulinzi au usalama wa kitaifa.

Idara inaruhusiwa pia kufichua taarifa binafsi inayolindwa kama mtu anakubali itolewe, utoaji ni lazima uwe una lengo la kuzuia au kupunguza kitisho kikali dhidi ya maisha au afya ya mtu au taarifa imewekwa wazi kwa umma kisheria.

Kifungu 51 cha Sheria ya Jeshi la Mpakani kinaeleza kwamba ufunuzi kwa kulingana na ruhusa fulani katika Sehemu 6 ya Sheria hiyo utafahamika kuwa ufunuzi unaoruhusiwa na Sheria hiyo kwa malengo ya Sheria ya Faragha.

Nyongeza, ufunuzi wa taarifa za Uhamiaji na Ulinzi wa Mipaka inaruhusiwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Mpakani kama ukifichua wakati wa ajira au huduma ya mtu aliyeaminiwa na Idara. Idara itahakikisha kwamba ufunuzi wowote unatii Sheria ya Faragha.

Idara inaruhusiwa pia kufichua taarifa binafsi inayokuwa taarifa inayokuwa imelindwa mara chache sana pale endapo sheria zilizohusu forodha kama Sheria ya Forodha na kanuni zake.

### Ufunuzi wa Kumbukumbu za Kubadili Mahali

Kumbukumbu za kuwasili na kuondoka kwa wasafiri kuja na kutoka Australia zinawekwa katika msingi wa data wa kumbukumbu za kubadili mahali. Zinaweza kufichuliwa kwa makusudi ya:

- Sheria ya Uhamiaji
- *Family Law Act 1975 (Sheria ya Familia 1975)*
- sheria za forodha au ushuru
- sheria za karantini au afya
- kutekeleza sheria
- *Education Services for Overseas Students Act 2000 (Sheria ya Huduma za Elimu kwa Wanafunzi wa Nje 2000)*
- sheria ya Jumuiya ya Madola, jimbo au wilaya yaliyoamurilwa, kama usimamiaji wa miradi ya wamiliki wa nyumba ya kwanza au miradi ya watoto na/au ustawi.


© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2020

### Ufunuzi kwa malengo ya kutekeleza sheria na kuhusika

Ufunuzi wa kawaida na Idara kwa malengo ya kutekeleza sheria na kuhusika (pamoja na shughuli za kutekeleza kufuata Masheria ya Uhamiaji na Uraia na shughuli za kutekeleza sheria za mashirika mengine ya kutekeleza) ni pamoja na:

- mashirika ya Australia na ya nchi za nje ili kutathmini na kutekeleza mahitaji ya tabia
- mashirika ya kutekeleza sheria ya Australia na nje na mashirika au tume ya upelelezi, Huduma za Polisi za Kawaida ya Kitaifa, Interpol, Kituo cha Kulenga Mpaka wa Kitaifa, CrimTrac, AusTRAC, tume ya masharti, tume ya bunge ya uchunguzi, baraza ya kimataifa na mamlaka ya uhamiaji wa nje, kutumbua au kuchunguza udanganyifu wa uhamiaji, maswala ya usalama wa kitaifa, au kuhusisha kwa tuhuma katika jinai ya vita au jinai kupinga ubinadamu
- Tume ya Australia kwa Ukamilifu wa Kutekeleza Sheria kusimamia *Law Enforcement Integrity Commissioner Act 2006 (Sheria ya Kamishina wa Ukamilifu wa Kutekeleza Sheria 2006)*
- ATO, DHS na mashirika mengine ya Jumuiya ya Madola au jimbo na wilaya kutambua mahali pa watu wanaofanya kazi kinyume na masharti ya viza za kufanya kazi
- AFP na majeshi ya polisi wa Australia kufahamu kutambua mahali pa watu wasio raia wasio halali
- Mkurugenzi wa Kuendesha Mashataka wa Serikali kushtaki makosa ya uhamiaji au uraia
- Serikali za nje kwa kuondoa mtu asiye raia asiye halali
- FWO, taasisi za elimu zilizoandikishwa, waajiri, watu waliofadhiliwa, wafadhili na watoaji wa kazi kusaidia kufuatia masharti ya viza na majukumu ya ufadhili, na kujulisha mifano ya kulazimisha ruhusa
- mashirika ya kutekeleza sheria pamoja na AFP kuhusu taarifa binafsi ya waombaji na wafadhili wa viza na chini ya mradi wa Wakimbizi na Kwenye Huruma, kutambua masuala yoyote ya kutekeleza sheria au usalama wa kitaifa.

### Ufunuzi na Idara kama shirika la kutekeleza sheria

Idara ni shirika la kutekeleza sheria kwa malengo fulani chini ya Sheria zifuatazo: the *Crimes Act 1914,* the *Criminal Code Act 1995,* the *Australian Nuclear Science and Technology Organisation Act 1987* (the ANSTO Act) and the *Independent National Security Legislation Monitor Act 2010* (*Sheria ya Makosa ya Jinai 1914, Sheria ya Kanuni ya Adhabu ya Jinai 1995, Sheria ya Shirika ya Sayansi ya Nyuklia na Teknolojia 1987* (Sheria ya ANSTO) na *Sheria ya Kuangalia kwa Uhuru Sheria ya Usalama wa Taifa 2010*), na inaweza kukusanya taarifa binafsi ili kufanya kazi na shughuli zake chini ya Sheria hizo.

### Ufunuzi mengine unahusiana na usimamiaji wa miradi

#### Uhakika msaada

Taarifa kuhusu watu wanaotoa Uhakika Msaada zitafichuliwa kwa Centrelink kusaidia kupatikana kwa dhamana iliyolipwa au kutambua na kupata tena madeni yaliyolimbikizwa.

#### Ajira, utoaji wa kazi na ustadi wa biashara

Idara inaweza kufichua taarifa kuhusu hali yako ya uhamiaji, ustahili wa kazi na aina na muda wa viza vyako kwa waajiri, watoaji wa kazi na vipande vya tatu wanaotumia huduma zako kupitia mipangilio ya utoaji wa kazi. Kwa mfano, wakati unapoomba kazi, Idara inaweza kufichua kwa mwajiri au mtoaji wa kazi juu ya ustahili wako kufanya kazi.

Idara inaweza pia kufichua taarifa kwa Idara na mashirika ya maendeleo ya kichumi ya jimbo na wilaya yanayosaidia wahamiaji wa ustadi wa biashara kufikia huduma za serikali ya maelezo ya biashara.

#### Mafunzo na elimu

Taarifa binafsi zinaweza kufichuliwa kwa:

- DFAT, Idara ya Tasnia na Idara ya Elimu kusaidia wanaotafuta kufanya mafunzo au kusoma nchini Australia
- Idara ya Ajira kuamua athiri yoyote ya sehemu ililyopendekezwa ya mahali pa kazi kwa soko la kazi ya Australia
- Idara ya Elimu na mamlaka iliyoagizwa inayotathmini sifa za nje kwa aina kadhaa ya viza
- taasisi za elimu zinazotoa mafunzo ya lugha ya Kiingereza chini ya Mradi wa Kiingereza kwa Watu wazima Wahamiaji
- Mamlaka za serikali kwa malengo ya kuwaongoza watoaji wa elimu.

#### Afya

Habari za afya yako na ya wanafamilia zilizotathminiwa kwa ombi lako la viza zinaweza kufichua kwa mashirika ya afya ya serikali na watoaji wa uganga kusaidia kuamua kama masharti ya afya imetimizwa kwa kupewa viza, kwa kufikiri kama masharti ya afya yanaweza kusamehewa, au kwa usimamizi wa hatari za afya ya umma.

#### Kuingia kwa Wakimbizi na Kwenye Huruma, na Ulinzi wa Upo-pwani

Idara inaweza kubadilishana taarifa binafsi za waingiaji wakimbizi na wa huruma na wafadhili (ikifaa) kwa watoaji wa huduma wa mkataba chini ya Huduma za Kutulia kwa Huruma.

Idara inaweza kutoa taarifa binafsi kuhusu watafute wa kimbilio na waombaji wa viza vya ulinzi au huruma kwa Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa Wakimbizi (UNHCR) kwa kusudi kwa kuhakikisha utambulisho, na maombi ya huruma au ulinzi.

Idara inaweza pia kutoa taarifa binafsi kwa Shirika la Mataifa kwa Uhamiaji kusaidia kutoa huduma zake.

#### Uzuizi

Idara inaweza kutoa taarifa binafsi kuhusu watu ambao wamo kizuizini cha uhamiaji kwa:

- mashirika ya ustawi wa jimbo na wilaya kuhusu mipango ya kizuizi mbadala, utunzaji kwa watoto wa chini wa umri wa miaka 18 wanako peke yao au ulezi kwa watu walioko kizuizi na ulemavu wa kimwili na kiakili
- huduma za magereza za jimbo na wilaya kusaidia uhamisho na kuhakikisha hali ya uhamiaji
- watoa huduma za usindikaji wa shughuli za eneo lililo mbali ya pwani, wakiunga mkono uhamisho
- mashule, madaktari na watoaji wa huduma za afya na ustawi, au washauri wa uhamiaji wanaotoa huduma kwako au kutathmini uchaguzi kukusaidia na familia yako kuondoka.

#### Ustawi na ulinzi wa watoto

Taarifa binafsi za watoto, na/au wazazi/walezi/watunzaji wa watoto, zinaweza kufichuliwa kwa mashirika ya ustawi na ulinzi wa watoto, mashirika ya ustawi wa watoto wa jimbo/wilaya, polisi ya jimbo/wilaya au mashirika mengine yanayohusika ya Serikali ya Australia ili:

- kupanga na kufuatia mipangilio ya utunzaji na ustawi ndani kizuizi cha uhamiaji na, au katika jumuiya
- kuchunguza mateso au kunyimwa yanayowezekana
- kusaidia mipangilio ya usafiri na hati.

Taarifa kuhusu watoto wanoingia Australia kwa ulezi zinaweza kufichuliwa kwa mashirika ya jimbo na ya wilaya, Mamlaka Muhimu ya Kuasili ya Australia na Kuasili Kati ya Nchi Australia.

#### Taarifa kwa balozi, tume kuu na balozi mdogo ili kupata hati za usafiri

Kama umepewa viza kwa sababu ya kuondoka au huna sababu ya kisheria kukaa nchini Australia unatazamiwa kuondoka. Kama humiliki au hupati hati ya usafiri katika muda wa kutosha ni kawaida kwa Idara kuomba viza kwa niaba yako. Hii inaruhusu mipangilio kwa kuondoka kwako kufanyika.

© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2020

Idara itatoa tu taarifa za mwisho zinazohitajika kwenye ubalozi unaofaa, tume kuu au balozi mdogo wa kufaa kusaidia kupata hati ya usafiri. Hiyo ni pamoja na jina lako, habari zilizo katika hati za pasi yako ya sasa au nyaraka nyingine za vitambulisho na habari za mawasiliano.

### Uraia

Idara inaweza kutoa taarifa binafsi nje ya vitambulisho binafsi kwa:

- halmashauri ya serikali za mitaa na mashirika mengine kwa kusudi la kuandaa na kufanya sherehe za uraia
- Ofisi ya Katibu Rasmi wa Gavana-Mkuu na Idara ya Waziri Mkuu na Baraza la Mawaziri kuangalia maombi kwa ya Australia honours
- Wabunge na Madiwani wa halmashauri ya serikali za mitaa kwa makusudi ya kuwakaribisha raia wapya katika jumuiya ya Australia.

### Utafiti wa uhamiaji

Taarifa za kibinafsi zinaweza kutumiwa kwa uchunguzi wa wateja wa sasa na wateja waliopita. Taarifa binafsi zinaweza kufichuliwa kwa mashirika mengine na wengineo wenye mkataba kwa makusudi ya utafiti, uchunguzi na uchambuzi kwa maendeleo ya siasa na/au mradi. Mikataba inazuia utumiaji kwa makusudi ya utafiti ulionenwa, na inahitaji kuharibika kabisa wakati umemaliza. Data zinazokusanywa na kutumiwa katika utafiti zinakuwa bila nafsi kabla kuruhusiwa kutolewa.

Taarifa binafsi zinaweza kufichuliwa kwa Ofisi ya Takwimu ya Australia kusaidia utafiti wa demografia kuhusu waingiaji wapya na uchambuzi ya miradi anuwai na matokeo ya makazi.

Taarifa kuhusu waingiaji wapya zinaweza kutolewa kwa mashirika ya jimbo na wilaya au mashirika ya huduma za wahamiaji kusaidia kupanga makazi au kutoa huduma za makazi.

## Matukio makuu ya kimataifa

Taarifa binafsi zinaweza kufichuliwa kwa mashirika ya Serikali ya Australia, pamoja na mashirika ya jimbo na wilaya, yanayokuwa na kazi ya kuratibu matukio makuu ya kimataifa, kama: mashindani makubwa ya michezo; mikutano ya wakuu wa nchi wa kimataifa; mikusanyiko au matamasha ya kimataifa ya kijamii, kitamaduni au kidini.

Idara inaweza pia kutumia na kufichua taarifa isiyo siri na mashirika ya Australia na kimataifa, na nchi nyingine, kusaidia mipango yako.

## Maelezo kuhusu siasa ya faragha ya Idara

Sera ya faragha ya Idara inapatikana kutoka tovuti ya Idara **https://www.homeaffairs.gov.au/access-and-accountability/our-commitments/privacy**

Siasa inakuwa ndani maelezo kuhusu:

- jinsi unavyoweza kufikia taarifa zako binafsi zenyewe zinazowekwa na Idara na kuomba zirekebishwe
- jinsi unavyoweza kulalamika kuhusu uvunjaji wa faragha na utaratibu wa Idara kufuatilia lalamiko.

## Ufunuzi wa taarifa zako kwa wapokezi wa ng'ambo

Idara inatumia makandarasi wa nje wa IT kupeleka na kuweka data, pamoja na watoaji wanapokuwepo ng'ambo.

Katika baadhi ya hali tunafichua taarifa binafsi kwa wapokezi wa ng'ambo. Mara nyingi mpokezi atakuwa nchi yako ya makazi ya kawaida au nchi ulipoondoka (isipokuwa umeshaweka maombi kwa ulinzi kupinga nchi zile na unasubiri tathmini ya maombi hayo kumalizika). Hiyo itakuwa pamoja na ufunuzi kwa mashirika ya ndege au mawakala wa usafiri kuhusu kushughulika abiria wa juu na viza kielektroniki.

Idara pia inabadilishana taarifa na nchi au mashirika ya kimataifa yanayokuwa na makubaliano ya kushirikiana taarifa na Australia pamoja na lakini bila mpaka na, Marekani, Uingereza, Kanada na Nyuziland. Ubadilishano huu wa taarifa unaweza kuhusiana kushirikiana biometrics (vitambulisho binafsi).

Kama kuna ulinganifu na vitambulisho wako binafsi, Idara inaweza kufichua data zako za historia za maisha yako, nakala za hati za kusafiria na zingine za utambulisho au taarifa kutoka hati hizi, hali yako ya uhamiaji (inayoweza kuwa pamoja na udanganyifu na makosa yoyote ya uhamiaji) na maelezo yoyote ya historia inayofaa ya jinai.

Kusudi ya ufunuzi huu ni kusaidia kuhakikisha nafsi yako na kuamua kama umeonyesha mashirika mengine kwa kutumia nafsi ileile na pamoja na madai sawa.

Kama unafanya ombi la viza ya mbali ya pwani la huruma au vya ulinzi kutumia madai kupinga serikali ya nchi fulani, Idara haitafichua taarifa zako binafsi kwa serikali ile, isipokuwa uko nchini Australia na:

- umeomba au umekubali kurudi katkia nchi hii, au
- umegundulika kutokuwa mtu ambaye Australia inadai kuwa na majukumu ya kulinda.

| | |
|---|---|
| *Ukurasa wa utangulizi* | **www.homeaffairs.gov.au** |
| *Simu ya kuuliza kwa jumla* | Piga simu **131 881** mnamo masaa ya kazi nchini Australia kuzungumza na operata (maelezo yaliyo rekodiwa yanapatikana nje ya masaa hayo). Kama upo nje ya Australia, tafadhali wasliana na balozi ya Australia ya karibu zaidi kwako. |


© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2020